TRA SACCOS LIMITED

CHAMA CHA USHIRIKA CHA AKIBA NA MIKOPO CHA MAMLAKA YA MAPATO TANZANIA

P.O BOX 63225 DAR ES SALAAM, TEL/FAX: +255 22 2864556
MOBILE: +255 712494312, +255 684 557070, +255 765 986455
WEBSITE: http://www.trasaccos.co.tz, EMAIL: info@trasaccos.co.tz

MKATABA WA MKOPO

Baina ya

TRA SACCOS LIMITED
(Ambaye ni MKOPESHAJI)

NA

Ndugu……..……..

Wa S.L.P……Mkoa wa……

simu…….
(Ambaye ni MKOPAJI)

.

Mkataba huu umetayarishwa na:
TRA SACCOS LIMITED

Mkataba huu umefanyika leo hii tarehe …… ya mwezi…….20….....

Kati ya

Chama cha Akiba na Mikopo cha Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA SACCOS LIMITED) taasisi ilioanzishwa kwa mujibu wa sheria za vyama vya Ushirika na Kanuni zake na anwani yake ni yake ni S.L.P 63225 Dar es Salaam (ambaye katika Mkataba huu atajulikana kama **MKOPAJI**) kwa upande mmoja.

Na

Ndugu …….. wa S.L.P ……. ……..(ambaye katika Mkataba huu utawahusisha na Warithi wa mali zake, wamiliki, wasimamizi na wadhamini ikibidi kwa upande mwingine)

KWA KUWA:

(i) **MKOPESHAJI** ambaye ni Chama Cha Akiba na Mikopo kilichoanzishwa kwa mujibu wa sheria.

(ii) **MKOPESHAJI** ambaye na amekubali kumpatia huduma ya mkopo **MKOPAJI**

(iii) **MKOPAJI** ni Mwanachama hai wa Chama Cha Akiba na Mikopo cha TRA SACCOS LTD.

(iv) **MKOPAJI** amekubali kupewa huduma ya mkopo kutoka kwa **MKOPESHAJI**.

KWA HIYO BASI MKATABA HUU UNASHUHUDIA KWAMBA:-

1. **MKOPESHAJI** ameamua kuweka fedha katika mzunguko ili asaidie wanachama wake hai kuinua, kustawisha na kuboresha hali zao za kiuchumi na kijamii.

2. **MKOPAJI** anatakiwa awe amerudisha mkopo na riba (interest) ndani ya kipindi alichoahidi kama ilivyoainishwa kwenye jedwali la urejeshaji mkopo ambalo limeambatanishwa katika mkataba na ni sehemu ya mkataba huu.

3. Mkopo huu utatolewa kwa kuingiza kiwango cha mkopo kilichoidhinishwa kwenye Akaunti ya Benki au Mtandao wa simu kwa namba ya **MKOPAJI**

4. **MKOPESHAJI** ndiye atakayepanga muda wa urejeshaji wa mkopo na anaweza kurekebisha riba pindi atakavyoona ni vyema kufanya hivyo kwa manufaa ya mfuko wa **CHAMA.**

5. **MKOPAJI** amekubali kulipa kwa kukatwa kwenye mshahara wake kiasi cha marejesho kwa wakati unaotakiwa kwa mujibu wa tarehe ya mshahara ya Mamlaka ya Mapato Tanzania jumla ya TZS_____yaani TZS_____kwa kila mwezi. Kushindwa kufanya hivyo kutamwezesha **MKOPESHAJI** kuchukua Hisa, Akiba na Pensheni ya Mkopeshwaji ili kurudisha deni lote pamoja na riba.

Endapo Hisa, Akiba na Pensheni za Mkopeshwaji hazitatosha kulipa deni lote pamoja na riba kama ilivyoelezwa hapo juu, basi wadhamini watatakiwa kulipa deni lote pamoja na riba iliyobakia na wakishindwa kulipa deni lote kama ilivyoelekezwa hapo juu, basi Hisa, Akiba na Pensheni/Mafao yao zitachukuliwa kulipa deni lote analodaiwa Mkopeshwaji pamoja na riba.

(b) ***Sehemu hii ijazwe na wanachama walio nje ya ajira ya Mamlaka ya Mapato***

MKOPAJI amekubali kulipa kiasi cha marejesho yanayotakiwa kwa mujibu wa makubaliano na Mkopeshaji jumla ya TZS_____yaani TZS_____kwa kila mwezi. Kushindwa kufanya hivyo kutamuwezesha Mkopeshaji kuchukua Hisa na Akiba.

MKOPAJI ametoa mali zifuatazo kama dhamana ya mkopo huu ambazo pamoja na hisa, akiba na pensheni za wadhamini zitatumika kulipa deni iwapo Mkopeshwaji atashindwa kulipa deni lake.

(i)_____

(ii_____

(iii) _____

Aidha dhamana hii pamoja na ile ya wadhamini itasimama pamoja. Mali hizi hazitahamishwa au kuuzwa na **MKOPAJI** au mdhamini/Wadhamini hadi deni litakapolipwa lote.

6. Endapo **MKOPAJI** atakiuka kulipa mkupuo wowote wa mtaji au riba kwa tarehe iliyopangwa , basi bakaa (Balance) yote itokanayo na mtaji na riba kama ilivyoonyeshwa katika mkataba huu ambayo itakuwa haijalipwa hadi kufikia tarehe ya ukiukaji huo itatakiwa ilipwe mara moja bila kujali kama tarehe ya kulipa mkopo huo kama ilivyoonyeshwa kwenye barua ya kukubaliwa ombi (**letter of offer**) itakuwa bado kufikiwa.

7. Kasoro yoyote itakayojitokeza kutokana na mkataba huu itasuluhishwa kwa njia ya majadiliano. Hata hivyo **MKOPESHAJI** anayo haki ya kuchukua hatua za kisheria ikiwa ni pamoja na kutaifisha mali wakati wowote pale ambapo usuluhishi wa kasoro hizo utashindikana kutatuliwa kwa njia ya majadiliano bila hata ya kwenda mahakamani.

8. Bila ya kuathiri masharti mengine katika mkataba huu, **MKOPAJI** anaweza kulipa mkopo pamoja na riba yake kutoka katika vyanzo vyake vingine vya mapato mbali na makato kutoka katika mshahara wake. Na hivyo atatakiwa kuandika barua inayoonyesha jinsi atakavyorejesha mkopo wake.

9. Endapo Mkopaji atashindwa kulipa mkopo wote au sehemu ya mkopo huo kwa sababu ya kuacha au kuachishwa kazi TRA SACCOS LTD ina haki ya kuchukua kutoka kwa mwajiri Mafao ya Mkopaji kulipia deni au sehemu ya deni lililo Baki.

10. Endapo Mtumishi aliyekopa atahama, au kuacha kazi na kujiunga na taasisi nyingine Mtumishi anatakiwa atoe utaratibu wa kuendelea kulipa deni hilo bila kuathiri makubaliano katika mkataba huu. Endapo atashindwa kutekeleza wajibu huu TRA SACCOS Ltd itawasiliana moja kwa moja na mwajiri wake mpya iwe Serikali, Taasisi Binafsi, Mashirika yasiyo ya Kiserikali n.k ili kuomba fedha anazodaiwa Mkopaji zikatwe na mwajiri na kuwasilishwa TRA SACCOS LTD

Mkataba huu umefikiwa na kushuhudiwa leo hii tarehe …… mwezi…… mwaka……...unavyoonyesha hapa chini kati ya **MKOPESHAJI** na **MKOPAJI.**
Umetiwa Muhuri na **TRA SACCOS LIMITED** na umepokelewa mbele yetu tarehe …….. mwezi…….. 20…….

Mkataba huu umewekwa na kusainiwa mbele yangu leo tarehe ……. Mwezi……. Mwaka 20……

JINA :(**WAKILI**)……JINA (**MKOPAJI**)……..……

ANUANI: ……..SAHIHI……

SAHIHI:…… TAREHE……

BANDIKA STEMPU YA USHURU

(Tamko hili ni lazima litolewe mbele ya Kamisha wa Viapo)

KAMATI YA MIKOPO KWA NIABA YA BODI

JINA LA MWENYEKITI : _____

SAHIHI _____

JINA LA MJUMBE :_____

SAHIHI _____

JINA LA KATIBU :_____

SAHIHI_____